Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

JIEPUSHENI NA KUNIULIZA, MPAKA NIWAFUNDISHE

8th Shawwal 1431
17th September, 2010

Volume 2, Issue 3

Mtayarishi: Imaam Ibn Rajab

Maandiko Ya Kuhusu Kuuliza Kupita Kiasi

Abu Hurairah (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alitoa khutba ambamo alisema: "*Enyi watu! Hajj ni waajib kwenu, kwahivyo tekelezeni Hajj.*"

Mtu mmoja akauliza, "Kila mwaka, Yaa Rasoolullaah?" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akanyamaza mpaka akaulizwa kwa mara ya tatu, kisha akasema: "*Nikisema, 'Ndio', itakuwa ni waajib (kila mwaka); lakini nyinyi hamutoweza kulitekeleza hilo.*"

Kisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema: "*Jiepusheni na (kuniuliza) mimi maadamu nawawachia; kwa hakika wale waliokuwepo kabla yenu waliangamizwa kwa masuali yao mengi na kutowaheshimu kwao Mitume wao. Ninapowaamrisha (mufanye) jambo (lolote), basi lifanyeni kiasi cha uwezo wenu; na ninapowakataza (katika) jambo, jiepusheni nalo.*" [al-Bukhaari na Muslim]

Amepokea Qataadah kutoka kwa Anas yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) alikuwa akiulizwa masuali kupita kiasi kuhusu mas'ala mengi, mpaka akakasirika sana siku moja, akapanda minbar na kusema, "*Leo hakuna atakaeniuliza kuhusu jambo lolote, isipokuwa nitamjibu.*" Mara mtu mmoja aliyekuwa na shaka iwapo mtu fulani ambaye aliyenasibishwa nae alikuwa ni babake wa halali alisema, "Ewe Mjumbe wa Allaah! Babangu ni yupi?" Mtume (صلى الله عليه وسلم) akamjibu, "*Hudhaafah ndiye babako.*" 'Umar, baada ya kutambua hasira alizokuwa nazo Mtume (صلى الله عليه وسلم) kutokana na masuali haya, alisimama na kusema: "Sisi tumetosheka na Allaah kwamba ni Mola wetu, na Uislamu kama ndiyo dini yetu, na Muhammad kama ndiye Mtume wetu. Twaomba hifadha kutoka kwa Allaah kutokana na *Fitnah*!"

Alipoitaja hadeeth hii, Qataadah vilevile alikuwa akiisoma Aya:

"Enyi mulioamini! Msiulize mambo ambayo mkidhihirishiwa yatakuchukizeni. Na kama mtayauliza, maadamu inateremshwa Qur'an mtabainishiwa. Allaah amesamehe hayo. Allaah ni mwingi wa kusamehe (na) Mpole sana. Watu wa kabla yenu waliyauliza, kisha wakawa wenye kuyakataa." [Al-Maa'idah 101-102]

Anas (رضي الله عنه) pia alieleza yakwamba kuuliza kwa yule mtu kumuhusu babake ndiko kuliko sababisha kuteremshwa kwa Aya ya hapo juu.

Makatazo Ya Kuuliza Masuali Kupita Kiasi

Kwahiyo, maswahaba walikatazwa kuuliza masuali yasokuwa na maana kama ilivyoashiriwa kwenye Aya ya hapo juu. Hii inathibitisha makatazo ya kuuliza kuyahusu yale ambayo kihakika muulizaji huwa hana haja nayo, kama kuuliza iwapo mtu yuko Motoni au Peponi, au iwapo babake wa halali ndiye yule ambaye aliyenasibishwa nae. Vilevile imekatazwa kuuliza masuali kwa njia ya vitisho, dhihaka, au istihzai, kama wafanyavyo wanafiki na wapotofu. Yenye kuhusiana na hayo ni yale ambayo Allaah ameyaficha kutoka kwa waja, kama kuhusu uhakika wa Wakati wa Mwisho, au umbile la

Yaliyomo

Jiepusheni na Kuniuliza Mpaka Niwafundishe 1- 4

roho. La ziyada ni kwamba, hii imewakataza Waislamu (katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم) wasiulize masuali ya kupita kiasi kuhusu ya halali na ya haramu, kwa kuhofia baadhi ya vikwazo huwenda vikateremshiwa Aya kuvihusu, kama kuulizia mas'ala ha Hajj, iwapo ni waajib kila mwaka au laa. Sa'd (رضي الله عنه) amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Kwa hakika aliye muovu zaidi miongoni mwa Waislamu ni yule mwenye kuuliza kuhusu jambo ambalo halijaharamishwa, lakini mara likaharamishwa kutokana na kuuliza kwake.*" [Bukhaari na Muslim]. Kwahiyo Muhaajiroon (wahamiaji) na ma-Answaar (wasaidizi) waliokuwa wakiishi Madeenah, na wale ambao nyoyo zao zilizokuwa thabiti juu ya Imaan, wao walikatazwa mambo ya kuuliza (bila ya dharura yoyote).

Masuali Yanayo Ruhusiwa

Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliuruhusu msafara wa mabedui kuuliza masuali (kwa min-ajil ya kusoma misingi ya Dini). Amepokea an-Nuwaas bin Sam'aan: "*Mimi nilikaa na* Mtume (صلى الله عليه وسلم) al-Madeenah kwa muda wa mwaka mmoja. Hakuna chochote kilichonizuiya na hijrah (ya kudumu) isipokuwa (ruhusa ya kuuliza) masuali. Kwani akiwa mmoja wetu atafanya Hijrah, hatopata tena fursa ya kumuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu

JIEPUSHENI NA KUNIULIZA, MPAKA NIWAFUNDISHE

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

suali lolote." [Muslim].

Amesema Anas: "Sisi tulikatazwa kumuuliza Mtume (صلى الله عليه وسلم) kuhusu mambo. Basi tulishangaa alipokuja mtu mmoja aliyekuwa na akili miongoni mwa mabedui. Alimuuliza masuali na tukawa twasikiza." (Muslim).

Baadaye, Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) walikuwa wakiuliza kuhusu baadhi ya mas'ala yenye umuhimu, kama kuhusu hukmu ya jambo litakalotokea, ili wapate kujua la kufanya hapo. Kwa mafano walikuwa wakiuliza: "Kesho tutapambana na adui yetu; na sisi hatuna hata visu. Twaweza kuwachinja (wanyama wetu kwa ajili ya chakula) kwa kutumia jiwe lenye makali, au(chombo chenye makali)?" [al-Bukhaari na Muslim].

Pia waliuliza iwapo wajisalimishe au wapigane na wale viongozi wapotofu ambao Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliwapasha habari yakwamba watakuja baada yake; aliuliza Hudhaifah kuhusu *fitan* (Fitna) zitakazotokea na jinsi ya kupambana nazo; na kadhaalika.

Sababu Za Kukatazwa

Katika hadeeth, Mtume (صلى الله عليه وسلم) alisema: "*Jiepusheni na (kuniuliza) mimi maadamu nawawachia; kwa hakika wale waliokuwepo kabla yenu waliangamizwa kwa masuali yao mengi na kutowaheshimu kwao Mitume wao.*

Hii inaashiriya yakwamba uulizaji usokuwa na umuhimu ni karaha na umekaripiwa. Baadhi ya watu wanadhani yakwamba hii ilikuwa ni makhsusi katika zama za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Wanatoa hoja yakwamba kwa kuendelea kuteremka *wahyi* juu ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) ingeliwezekana kwa jambo ambalo halikuwa limekatazwa likatazwe, au jambo gumu kutekeleza lifanywe kuwa ni waajib. Hali hii haikuwa hivyo baada ya kufa kwake Mtume (صلى الله عليه وسلم).

Hatahivyo, kuna sababu nyengine ya kukatazwa: wasiwe na pupa, lakini badala yake na wausubiri *wahyi* wa Qur'aan, ambao utakaoleta ubainifu wa wazi katika kila kitu ambacho huwenda wakakiulizia baadae. Yote ambayo Waislamu wanayohitaji kuyajua kuihusu Dini yao yamebainishwa na Allaah kwenye kitabu chake Kitukufu; na Mtume (صلى الله عليه وسلم) akayafikiliza. Kwahivyo hapana haja ya uulizaji zaidi ya hayo; Allaah anajua zaidi ni mas'ala yapi yenye kumsaidia mja wake, ni yapi yatakayompa uongofu, na ni yapi yatakayompa faida. Kwa hakika, Allaah (سبحانه وتعالى) atayaletea ubainifu haya, hata kama wao hawayaulizii, kama alivyosema (سبحانه وتعالى): **"Allaah anakubainishieni ili msipotee."** [an-Nisaa' 4:176].

Kwahivyo, hapana haja kuuliza kuhusu jambo kabla ya kutokea haja yake. Katika hali kama hii, mtu anatakiwa ayafahamu yale ambayo Allaah na Mtume wake wamekwisha kutueleza, kisha ufuate hayo na uyatendee kazi.

Baina ya Uulizaji Na Kumtwi'i Allaah Na Mtume Wake

Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema katika hadeeth hii: "*Ninapowaamrisha (mufanye) jambo (lolote), basi lifanyeni kiasi cha uwezo wenu; na ninapowakataza (katika) jambo, jiepusheni nalo.*"

Kwa haya, Mtume (صلى الله عليه وسلم) anaashiria yakwamba kujishughulisha na kuzifuata amri zake, na kujiepusha na makatazo yake, kutamfanya mtu awe na kazi kubwa ya kuuliza masuali. Waislamu na wajishughulishe na mas'ala ambayo yaliyozungumzwa na Allaah na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم) peke yake, wajipinde katika kuyafahamu, wajisalimishe kwayo, wang'ang'ane katika kuyatekeleza maamrisho kadiri ya uwezo wao, na kupambana kujiepusha na yaliyoharamishwa. Huu ndio mwendo wa Maswahaba wa Mtume (صلى الله عليه وسلم) na wale waliowaandama wao kwa *Ihsaan* (kwa wema) kwa kutafuta 'ilmu yenye manufaa kutoka kwenye Kitaab na Sunnah. Anaposikia amri au makatazo, msikilizaji na asifanye dhana kuhusu mas'ala ambayo huwenda yakatokea au yasitokee. Ikiwa atafanya, atakuwa ni mwenye kuwajibika kwenye makatazo katika hadeeth, na ataonyesha udanganyifu katika kufuata maamrisho.

Mtu mmoja alimuuliza Ibn 'Umar kuhusu kulibusu Jiwe Jeusi. Ibn 'Umar (رضي الله عنه) akamjibu, *"Mimi nilimuona Mtume* (صلى الله عليه وسلم) *akilibusu na akiliguса",* Yule mtu akasema, "Jee ikiwa nimesukumwa mbali nalo? Jee ikiwa nimeshindwa nguvu (na kundi la watu)?" Ibn 'Umar (رضي الله عنه) akamjibu: "Hiyo 'Jee ikiwa' yako iwache kwenu Yemen. Mimi *nilimuona Mtume* (صلى الله عليه وسلم) *akilibusu na akiligusa.*" [al-Bukhaari]. Ibn 'Umar alimaanisha yakwamba kujihusisha kwako kuwe ni kumfuata Mtume (صلى الله عليه وسلم) peke yake; hapana haja ya kudhania uzito au kutoweza kufanya jambo kabla halijatokea, kwa sababu inadhoofisha azimio la kufikia malengo. Kwa hakika, *fiqh* (ufahamu) ya Dini na uulizaji kuhusu 'ilmu husifiwa iwapo yatafanywa kwa ajili ya kuyatendea kazi peke yake, wala si kwa ajili ya mijadala na ugomvi. Amesema Ibn Mas'ud (رضي الله عنه): "Utafanyaje *fitnah* (mikasa) ikitokea juu yako, ikamsababisha barobaro awe Mzee, na mtoto awe barobaro? Watu wataishika kama Sunnah; na iwapo itatekelezwa kwa njia tafauti siku moja, itasemwa, hii ni Munkar (karaha)."

Aliulizwa, "Yatatokea lini haya?" Akajibu, "Mutakapokuwa na watu waaminifu wachache, lakini viongozi wengi; mutakuwa na *ma-Fuqahaa* (watu wenye ufahamu) wachache, lakini wasomaji wengi; *fiqh* itafanyiwa utafiti kwa isiyokuwa Dini; na Ulimwengu utatafutwa kwa 'amali ya akhera.

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

JIEPUSHENI NA KUNIULIZA, MPAKA NIWAFUNDISHE

Vilevile, Maswahaba wengi na wafuasi wao walikuwa hawapendi kuulizwa masuali yenye kuhusu mambo kabla hayajatokea kabisa; na walikuwa hawajibu masuali kama hayo. Yoyote mwenye kuipita njia kwa ajili ya kutafuta 'ilmu kulingana na mpangilio tuloutaja, atalifahamu jawabu la matukio mapya mengi, kwa sababu yameegemezwa juu ya misingi hii. Na kupita juu ya njia hii ni lazima yafanywe kwa kuwafuata ma-Imaam (wanavyuoni wakubwa) ambao Ummah unawakubali kuhusiana na uongofu na utambuzi wao, kama ash-Shaafi'ee, Ahmad, Is-haaq, Abu 'Ubayd, na kila mwenye kufuata njia yao. Yoyote mwenye kufuata njia isiyokuwa hii atasumbuka ashindwe na kuangamia, ajichukulie yasiyoruhusiwa kwake, na ajiepushe na anayowajibika kuyafanya.

Mzizi wa suala lenyewe ni kwamba, kwa huko kuuliza, niya ya mtu inatakikaniwa kuwa ni kwa ajili ya Uso wa Allaah (سبحانه وتعالى), kujikurubisha Kwake kwa kuyajua Aliyoyateremsha kwa Mtume Wake, kupitia juu ya njia yake na kutekeleza kulingana nayo, na kuwalingania viumbe kwenye hayo. Yoyote mwenye kufanya hayo, Allaah humpa *fiqh*, na humlinda, auzindue moyo wake, na kumfunza yale ambayo asoyajua kwa upande mwengine. Kisha atakuwa ni mmojawapo wa wale waliosifiwa kwenye Kitabu kwa 'ilmu yao. Amesema Allaah (سبحانه وتعالى):

"Kwa hakika wanaomwogopa Allaah miongoni mwa waja Wake ni wale wataalamu (wanavyuoni)."

Sawa na hayo ni msemo wa wanavyuoni wa kale: "Uchaji Mungu ni dalili itoshayo ya 'ilmu ya mtu, na uzembe mbele ya Allaah ni dalili itoshayo ya ujinga wa mtu."

Kumtwi'i Allaah Na Mtume Wake Kwa Mukhtasar

Tumehitimisha yakwamba mtu na aelekeze juhudi zake kwenye kuyafahamu maneno ya Allaah na yale ya Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم) badala ya kujishughulisha na mas'ala mengi ambayo hayakujadiliwa kwenye Kitaab cha Allaah wala Sunnah za Mtume (صلى الله عليه وسلم). Yoyote mwenye kuyafanya hayo, akitafuta kwa hayo aafikiane na maamrisho na kujiepusha na makatazo, atakuwa ni miongoni mwa wenye kutekeleza amri za Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye hadeeth hii.

Kwa upande mwengine, yoyote ambaye, badala ya kushughulika na kuyafahamu aloyateremsha Allaah kwa Mtume Wake (صلى الله عليه وسلم), anaelekeza juhudi zake kwenye kuleta mas'ala ambayo yanaweza au yasoweza kutokea, akitarajia jawabu iliyotegemezwa juu ya Rai tupu, yuko kwenye hatari ya kupata upinzani na hadeeth hii, kufanya yale yanayokataza, na kujiepusha na inayoamrisha.

Unatakiwa ujue yakwamba mambo mapya mengi, ambayo hayana misingi kwenye Kitaab na Sunnah, hutokea tu kutokana na ukosefu wa kujisalimisha na amri za Allaah na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم). Iwapo katika hali yoyote, mtu anauliza kuhusu hukmu za Allaah kuhusiana na hayo na akayafuata, na aliyoyakataza kuhusiana nayo akajiepusha nayo, kisha tukio hili likatokea ndani ya mipaka ya Kitaab na Sunnah. Lakini mtu akifanya jambo kulingana na Rai yake na mapendeleo ya nafsi yake, basi mambo mengi yatokeayo yatakwenda kinyume na Sheriya za Allaah. Huwenda ikawa mara nyengine ni vigumu kwa mtu kupata hukmu za matukio haya kwenye Kitaab au Sunnah, kwa sababu ya kuwa mbali kwao na wao.

Kwa mukhtasar, mtu ni lazima atekeleze kulingana na aliyoyaamrisha Mtume (صلى الله عليه وسلم) kwenye hadeeth hii, na ajiepushe na aliyoyakataza Mtume (صلى الله عليه وسلم). Yoyote mwenye kujishughulisha na haya, badala ya mambo mengine, ataokolewa kwenye maisha haya na ya kesho Akhera. Na yoyote mwenye kufuata mawazo yake ya ghafla yanayomjia badala ya haya basi atawajibika na Onyo la Mtume (صلى الله عليه وسلم); na kwamba atakuwa anajifanya kama Watu Wa Kitabu, ambao walioangamizwa kwa ajili ya uulizaji wao wa kupita kiasi na kuwakaidi Mitume wao.

Mkazo Juu Ya Kujiepusha Na Makatazo

Katika hadeeth ya hapo juu, amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): "*Ninapowaamrisha (mufanye) jambo (lolote), basi lifanyeni kiasi cha uwezo wenu; na ninapowakataza (katika) jambo, jiepusheni nalo.*"

Baadhi ya wanavyuoni baada ya kuliangazia suala zima, wamekatikiwa yakwamba makatazo ni yenye nguvu zaidi kuliko maamrisho, kwa sababu hakukubakia lenye kuruhusu kwenye makatazo, haliyakuwa amri iko kwenye viwango vya uwezo wa mtu. Haya yamepokewa kutoka kwa Imaam Ahmad. Wengine wanasema kama hivyo: "Mambo mema hufanywa na wote wema na waovu; lakini maovu hayaepukwi isipokuwa na walio *siddeeq* (wakweli kabisa)."

Abu Hurairah amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Jihifadhi nafsi yako na Makatazo; ndipo utakapokuwa mfanya ibada wa kihakika miongoni mwa watu.*" [Ahmad, at-Tirmidhee, Ibn Maajah na wengineo]. Ni wazi yakwamba yaliyosemwa kuhusu fadhla za kujiepusha na makatazo juu ya utekelezaji wa vitendo vya utwi'ifu inahusu vitendo vya khiyari vya utwi'ifu peke yake. Utekelezaji wa kitendo cha lazima (waajib) ni muhimu zaidi kuliko kuepuka makatazo; hilo la awali ni tendo la kuungama lenye kujitosheleza,

JIEPUSHENI NA KUNIULIZA, MPAKA NIWAFUNDISHE

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 3)

haliyakuwa hilo la baadae ni tendo la kutengua lenye kustahili kuepukwa na, kwahivyo, halihitaji Niya kama yaliyo waajib. Zaidi ya hayo, kujiepusha na baadhi ya vitendo huwenda kukampeleka mtu kwenye ukafiri, kama vile kujiepusha kuitamka Shahaadah au kutoka kwenye utekelezaji wa nguzo za Uislamu. Mambo kama hayo sivyo yalivyo kwenye hali ya kutekeleza makatazo, kwani utekelezaji huwo haulazimishi ukafiri. Kwa kuhitimisha, kujiepusha na makatazo – hata kama ni mambo madogo, ni bora kuliko kutekeleza vitendo vya khiyari vya utwi'ifu kwa wingi, kwani la kwanza ni waajib, haliyakuwa jenginelo ni la khiyari.

Uwezo: Kuhusiana na sehemu hiyohiyo ya hadeeth (ya Abu Hurairah), baadhi ya wanavyuoni wa baadae wameashiria yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema hivyo kwa sababu ya kuafiki maamrisho hakuwezi kutokea isipokuwa kwa kitendo cha (kuungama), ambayo hutegemea masharti na sababu fulani ambazo mtu asoweza kutekeleza bila ya kupatikana hizo. Kwahiyo iko chini ya mipaka ya uwezo kama ilivyo amri ya Allaah ya kuwa na *taqwaa*. **"Mcheni Allaah muwezavyo, (mwisho wa jitihada yenu)** [at-Taghaabun 64:16].

Na akasema Allaah (عزّ وجلّ) **"... na Allaah amewawajibisha watu wafanye Hijja katika nyumba hiyo; yule awezae kufunga safari kwenda huko ..."**[Aali 'Imraan 3:97].

Amma kuhusu makatazo, yanayo tarajiwa ni kwamba yanafanywa, na hiyo ndiyo asli (kwamba yanafanywa). Kwahivyo malengo ya kutoyafanya inabaki kuwa ni hukmu, na hili lawezekana, kwani haitegemei uwezo. Na bado kuna matatizo kwenye mjadala huu. Iwapo ulinganizi wa kwenye kitendo kiovu umemzidi mtu nguvu, na akakosa kuwa na subra yenye kuwajibika kujiepusha kuitekeleza kama ana uwezo, inakuwa ni wajibu kwake kujitahidi kadiri ya uwezo wake ili ajiepushe. Kwa baadhi ya watu, jambo hili (la kujiepusha na maovu) ni gumu sana kwao kuliko kufanya jambo jema. Kwa ajili hii kuna watu wengi wenye kufanya vitendo vya utwi'ifu, lakini hukosa nguvu za kujiepusha na baadhi ya makatazo. Ukweli wa yote haya ni kwamba Allaah hamkalifishi mtu kwa jambo asilo na uwezo nalo; na Yeye (سبحانه وتعالى) amewasamehe watu katika uwajibikaji mwingi kwa ajili ya dhiki itakayowapata tu, akawapa tahfifu kutokana na rehma juu yao. Amma kuhusu makatazo, mtu hafai kuhalalisha kuyafanya kutokana na nguvu za ushawishi au kuyapendelea. Bali, anatakiwa mtu kujiepusha nayo kwenye hali zote. Na lolote ambalo Allaah (سبحانه وتعالى) alililoliruhusu katika vyakula vya haramu ni kwa hali za dharura peke yake, kwa ajili ya kuhifadhi maisha, na wala si kwa ajili ya starehe au kuyatosheleza matanio. Hapa mtu atazinduka kwa aliyoyasema Imaam Ahmad (**رحمه الله**), yakwamba makatazo ni makali zaidi kuliko maamrisho.

Mtu Asipoweza Kutekeleza Maamrisho Kabisa

Hadeeth hii inazidi kutupa dalili yakwamba yoyote mwenye kuona uzito katika kufanya yote hayo aliyoamrishwa, lakini akawa anaweza kufanya baadhi yake, kisha akayafanya aliyokuwa na uwezo nayo. Hii ni kulingana na mas'ala tafauti, kama kujitwahirisha kwa mfano. Mtu akiweza kuyafanya baadhi ya mambo lakini akashindwa kuyafanya mengine kutokana na ukosefu wa maji au matatizo na baadhi ya viungo vyake, atafanya yale aliyo na uwezo nayo, na atekeleze *tayammum* kwa yaliyosaliya. Ni sawa iwapo hali imehusu *kutawadha* au *ghusl* (kulingana na wanavyuoni wengi). Ni sawa na swala, kwani yoyote mwenye kuona uzito kutekeleza mambo ya kuwajibika ya swala haliyakuwa amesimama, basi ataswali kwa kukaa. Ikiwa hilo litakuwa ni uzito kwake, basi ataswali haliyakuwa amelala. Katika *swaheeh al-Bukhaari*, 'Imraan bin Hussein amepokea yakwamba Mtume (صلى الله عليه وسلم) amesema: "*Swali (haliyakuwa) umesimama, iwapo huwezi, basi (swali haliyakuwa) umekaa, iwapo huwezi, basi (swali haliyakuwa) umelala kwa ubavu.*"

Ikiwa yote haya ni uzito tu, au ikiwa mtu hawezi kutumia viungo vyake kabisa, basi ataswali kwa kuashiriya kwa macho yake na kwa Niya; hakuruhusiwa asiswali ... Allaah yanamueleya zaidi.

P. O. Box 85477,
Mombasa,
Kenya.

E-mail: info@qssea.net

QSS (E.A)

جمعية القرآن والسنة في شرق إفريقيا

Tuko katika Tovuti
http://www.qssea.net